



Hakika zitatokea fitina, kisha tambueni kuwa fitina ya aliyekaa ndani inanafuu kuliko anayetembea, na anayetembea ndani yake inanafuu kuliko anayeikimbilia,

Kutoka kwa Othman As Shaham, amesema: Niliondoka mimi pamoja na Farqad As Sabakhi kwenda kwa Muslim bin Abii Bakara naye akiwa katika mji wake, tukaingia kwake na tukasema: Hivi uliwahi kumsikia baba yako akisimulia hadithi yoyote kuhusu fitina? Akasema: Ndiyo, Nilimsikia Abuu Bakra radhi za Allah ziwe juu yake akihadithia, akasema: Alisema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Hakika zitatokea fitina, kisha tambueni kuwa fitina ya aliyekaa ndani inanafuu kuliko anayetembea, na anayetembea ndani yake inanafuu kuliko anayeikimbilia, tambueni itakapoteremka au ikatokea basi atakayekuwa na ngamia basi na amfuate ngamia wake, na atakayekuwa na mbuzi basi na amfuate mbuzi wake, na atakayekuwa na ardhi basi na aende katika ardhi yake", anasema, akasema mtu mmoja: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wasemaje ikiwa mtu hana ngamia wala mbuzi wala ardhi? Akasema: "Basi achukue panga lake na apige upande wa makali yake katika jiwe, kisha aokoze akiweza kuokoka, ewe Allah je nimefikisha? ewe Allah je nimefikisha? ewe Allah je nimefikisha?" Akasema: Akasema mtu mmoja: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wasemaje endapo nitalazimishwa mpaka nikapelekwa katika moja kati ya safu mbili, au moja kati ya makundi mawili, mtu mmoja akanipiga kwa panga lake, au ukanilenga mshale ukaniua? Akasema: "Yeye ndiye atakayebeba dhambi zake na dhambi zako, na atakuwa miongoni mwa watu wa motoni".

[Sahihi] [Imepokelewa na Imamu Muslim]

Othman Ash Shaham na Farqad As-Sabakhi walimuuliza Muslim mtoto wa Swahaba mtukufu Abuubakra radhi za Allah ziwe juu yake: Je alisikia kutoka kwa baba yake hadithi kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika fitina na vita itakayotokea baina ya waislamu? Akasema: Naam, alieleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kwamba itatokea fitina baada ya kifo chake, na fitina hii aliyekaa na kughafilika nayo ni bora kuliko anayetembea ndani yake, na anaitafuta pasina kujua, na anayetembea ndani yake ni bora kuliko anayekwenda mbio kuiendea na kuitafuta na kushiriki ndani yake. Kisha akaelekeza Mtume rehema na amani ziwe juu yake itakayeshuka na kufika fitina katika zama zake na kwake kukapatikana upenyo atakaokimbilia; atakayekuwa na ngamia anayechunga basi aifuate ngamia yake, na atakayekuwa na mbuzi anayechunga basi amfuate mbuzi wake, na atakayekuwa na ardhi na shamba basi aende shambani kwake. Bwana mmoja akasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hivi wasemaje kwa mtu ambaye hatokuwa na makimbilio kama

ngamia wala mbuzi wala shamba? Akasema: Basi aende akachukue silaha yake aipige na ailainishe, kisha akimbie na ajinusuru yeye na mwanaye ikiwa ataweza kuokoka. Kisha akataka ushuhuda rehema na amani ziwe juu yake mara tatu, akasema: Ewe Allah je, nimefikisha? Ewe Allah je nimefikisha? Ewe Allah je nimefikisha?. Bwana mmoja akasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wasemaje ikiwa nitalazimishwa kushiriki pamoja na safu moja, au moja kati ya makundi mawili, akanipiga mtu kwa panga lake, au mshale ukanilenga ukaniuwa?. Akasema: Atarudi na madhambi yake na madhambi ya aliyemuwa, na siku ya Kiyama atakuwa miongoni mwa watu wa motoni.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/66383>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

